## 4.2 KISWAHILI (102)

### 4.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

1. Hii ni ripoti rasmi.

Mtahiniwa ajikite kwenye vipengele viwili vikuu vya uandishi wa ripoti; **maudhui** na **muundo**.

**(a) Muundo**

(i) Hii ni ripoti ya uchunguzi. Yafuatayo yazingatiwe:

(I) Anwani: mf. RIPOTI YA UCHUNGUZI KUHUSU VYANZO VYA ONGEZEKO LA VISA VYA WANAFUNZI KATIKA ENEO LA TELEKEZA KUACHA SHULE

(II) Utangulizi
Ubainishe:

(i) Suala linaloshughulikiwa.

(ii) Kiini/Kusudi/Hadidu za rejea
Aelezee kwa muhtasari malengo ya utafiti, kusudi la kuteuliwa kwa kamati/jopo hili.

(iii) Mbinu za utafiti/uchunguzi
Aeleze jinsi alivyopata habari kuhusu mada hii. Mbinu za kupata habari hizi ni kama vile hojaji, mahojiano
Anaweza pia kutaja majina ya wanajopo.

**(b) Mwili**
Hapa ndipo mtahiniwa atakapojadili hoja zinazohusiana na mada. Kila hoja iandikwe kama kichwa kidogo. Kwa mfano:

(a) Umaskini

Matokeo ya utafiti yabainike vyema.

**(c) Hitimisho na mapendekezo**
Mtahiniwa ajumuishe hoja/mawazo yake kuhusiana na mada, kisha atoe mapendekezo kuhusiana na namna ya kusuluhisha tatizo hili. Anaweza pia kupendekeza utafiti mwingine ufanywe kuhusu changamoto hii.

**(d)** Sahihi, jina, cheo, tarehe
Hiki ndicho kipengele cha mwisho kabisa cha kimuundo.
Aliyeandika ripoti ajitambulishe. Jina na sahihi ya mwenyekiti wa jopokazi hili linaweza pia kuandikwa pamoja na la katibu.

**Maudhui**

Baadhi ya hoja zinazoweza kujitokeza ni:

(i) Umaskini unaoweza kusababisha ukosefu wa karo na mahitaji mengine ya kimsingi hivyo kuwafanya wengine kutohudhuria shule na hatimaye kuacha.

(ii) Ukosefu wa vielelezo katika jamii - wanafunzi kukosa msukumo/motisha ya elimu

(iii) Tamaduni na desturi hasi, kwa mfano kuozwa mapema

(iv) Ajira ya watoto - wengine kutoka ili kufanya kazi

(v) Hamahama za wazazi kutoka sehemu moja hadi nyingine

(vi) Uyatima unaowapagaza baadhi ulezi, hivyo kuacha shule.

(vii) Dhiki za kisaikolojia kutokana na majanga au misiba, hivyo kutokuwa na hamu ya kuendelea na masomo
(viii) Mimba nje ya ndoa kuwafanya wasichana kutoendelea na shule
(ix) Uraibu wa dawa za kulevya - wengine kuwa walanguzi
(x) Kutopata mwongozo bora kutoka kwa wazazi kuhusu umuhimu wa elimu
(xi) Uongozi dhaifu shuleni - usimamizi wa shule kutofuatilia nidhamu na hali ya wanafunzi. Baadhi huzembea shule, hujificha njiani na baadaye kurudi nyumbani. Hatimaye huacha shule.
(xii) Tatizo la usalama katika baadhi ya maeneo; baadhi ya wanafunzi huweza kutekwa nyara na kuachishwa shule.
(xiii) Hali duni ya miundomsingi shuleni huweza kuwafanya baadhi kutovutiwa na shule.
(xiv) Ukosefu wa usalama wa chakula (kutojitosheleza kwa chakula). Baadhi ya shule hazina mpango wa kuwapa watoto/wanafunzi chakula, wengine huacha shule kwa sababu ya njaa.
(xv) Kunyanyaswa kimapenzi na walimu/walezi huwatia unyanyapaa na kuwafanya kuacha shule.
(xvi) Magonjwa kama vile ukimwi huwafanya wengine kutokubaliwa na wenzao na kulazimika kuacha shule.
(xvii) Vivutio kutoka kwenye mazingira, kwa mfano baadhi kuvutiwa na watalii na kuhiari kuhusiana nao kimapenzi badala ya kuendelea na masomo
(xviii) Umbali baina ya wanakoishi na shule
(xix) Kukosa vifaa (sodo) vya kukabiliana na hedhi
(xx) Matatizo ya kinidhamu. Baadhi kufukuzwa kutoka shule moja hadi nyingine, hatimaye kuacha shule kwa kujiona wasiofaa
(xxi) Migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyowafanya baadhi kutokubaliwa katika maeneo mengine na hatimaye kuacha shule.
(xxii) Wengine, kwa kutofanya vyema katika masomo, hukata tamaa na kuhiari kuacha shule.

**Mapendekezo**

Baadhi ni:

(i) Kuanzisha hazina ya kutoa udhamini wa masomo
(ii) Kustawisha idara za ushauri na uelekezaji
(iii) Mradi wa kuwapa wanafunzi chakula shuleni
(iv) Wazazi/walezi kuhamasishwa dhidi ya kuwaoza watoto wao mapema
(v) Kampeni za kuwapa wasichana sodo ziimarishwe
(vi) Kuanzisha vyuo vya ufundi ili wasiomudu masomo ya kiakademia wasajiliwe huku na kujiendeleza kielimu.
(vii) Tafiti zaidi zifanywe ili kubainisha kwa mfano, vyanzo vya wazazi kuwaoza watoto mapema.

**Tanbihi**

Mtahiniwa anaweza kutoa mifano kutoka shule za msingi au shule za upili.

2. (i) Tamasha za muziki hukuza utangamano miongoni mwa vijana kwani hukutana kutoka tamaduni tofautitofauti.
(ii) Ni njia ya kukuza na kuendeleza vipawa.
(iii) Huwapevusha akili kutokana na mada wanazopewa kujadili, hasa katika hotuba fupi za hadhara.

(iv) Ni njia ya kuwafanya vijana kuhifadhi utamaduni wao kupitia nyimbo, maghani na mashairi teule.

(v) Huwafunza stahamala/heshima kwa tamaduni nyingine.

(vi) Vijana huweza kunufaika kutoka tamaduni nyingine, kwa kuiga mema yanayofumbatwa na tungo ambazo zinawasilishwa.

(vii) Hukuza uzalendo. Vijana hujifunza kufurahia utamaduni wao kupitia nyimbo na ngoma.

(viii) Huimarisha uwajibikaji. Wapo vijana ambao ni viongozi wa makundi yao, pia vijana hujifunza kutangamana kwa kuweka mipaka ya kimahusiano.

(ix) Huwapa vijana fursa ya kujieleza, hivyo kupata kujiamini/ukakamavu.

(x) Huvyaza walumbi miongoni mwa vijana, kupitia hotuba.

(xi) Hukuza fani mbalimbali miongoni mwa vijana. Kwa mfano uigizaji, uimbaji. Vijana huweza kutumia fani hizi kujipatia riziki.

(xii) Huimarisha uhusiano kati ya vijana na walimu wao, hasa wakati wa kufanya mazoezi kabla ya mashindano.

(xiii) Ni njia ya kuwatayarisha vijana kwa ulimwengu wa ushindani. Mashindano yanayoandaliwa huwafanya wanafunzi kutafuta mikakati ya kujiboresha. Wanaweza kuitumia mikakati hii katika maisha yao ya baadaye.

(xiv) Hukuza unyenyekevu. Vijana hujifunza kukubali ushindi.

(xv) Ni nyenzo bora ya kupalilia mtazamo chanya kuhusu baadhi ya masomo kama vile ushairi. Wanafunzi hujitambulisha nayo zaidi.

**Tanbihi**

Mtahiniwa si lazima ajikite kwenye mazingira ya shule. Anaweza kujadili tamasha zozote za muziki.

3. Mtahiniwa abuni kisa kinachodhihirisha maana ifuatayo:
Mtu asipolirekebisha jambo mapema hatimaye tatizo litakuwa kubwa na kumhitaji kutumia nguvu/rasilimali nyingi kulitatua. Huweza pia kumshinda kulirekebisha kutokana na uchangamano walo.

Hali zifuatazo zinaweza kujitokeza:

(i) Mhusika aanze mazoea ya kuchelewa kazini, apuuze, tatizo hili baadaye kuwa sugu, hata aachishwe kazi.

(ii) Mzazi akose kumrekebisha mwanawe mtundu na baadaye mwana huyu aharibike, mzazi ateseke kuyatatua matatizo ya mwana.

(iii) Mhusika apatwe na dalili za ugonjwa fulani, azipuuze na hatimaye kulazimika kutumia pesa nyingi kuutibu ugonjwa uliomlemaza zaidi.

(iv) Mwashi/mwenye nyumba aone dalili ya udhaifu kwenye jengo, akose kulirekebisha na hatimaye jengo hilo kuanguka; pengine hata kuwahasiri watu; na mwenye nyumba kulazimika kulipa fidia.

(v) Mhusika aone/akisie dalili za ujambazi kutoka kwa jirani yake. Apuuze, asiwaarifu polisi. Baadaye jirani huyu kuwaibia na wakazi kulazimika kutafuta namna ya kufidia mali iliyopotea.

(vi) Mwanafunzi awe mvivu, ahimizwe na mwalimu kusomea mtihani, apuuze na kuishia kufanya vibaya katika mtihani, pengine hata anarudia mtihani.

(vii) Mhusika aliyeona ana tatizo dogo, akagundua umuhimu wa kulitatua, na hatimaye kuepuka janga

(viii) Uongozi uone udhaifu katika miundomsingi, upuuze, na barabara kuishia kutwaa mashimo yanayotinga usafiri.

(ix) Raia waanze kukata miti, wapuuze umuhimu wa kupanda mingine, na kuishia kuteseka kwa kuyapujua mazingira yao. Kwa mfano, kunaweza kuwa na joto kali, kukosa kuni, n.k.

**Tanbihi**

(i) Ufa (tatizo) sharti ujitokeze, kwa mfano utovu wa nidhamu.
(ii) Mhusika abaini/abainishiwe kuwa tatizo lipo.
(iii) Akose kushughulikia hali/ashughulikie hali.
(iv) Ateseke kukabiliana na hali nzito zaidi/ahasirike, au
(v) Aweze kujirekebisha na kuepuka madhara makubwa zaidi.
(vi) Mtahiniwa anaweza pia kuwasawiri wahusika wawili; mmoja aliyerekebisha jambo mapema, akaneemeka, na mwingine aliyekosa kurekebisha, akahasirika.

4. (i) Mtahiniwa abuni kisa kinachoanza na kuafikiana na kauli aliyopewa.
(ii) Kisa kionyeshe tukio ambalo linasababisha hali ya **furaha** na **majonzi/huzuni.**
(iii) Kibainishe wahusika wawili:
(a) msimulizi
(b) mhusika anayetazamwa
(iv) Kisa kinaweza pia kuwa na wahusika zaidi ya wawili, pengine mmoja anayemwathiri yule aliye na machozi ya furaha na majonzi.

Hali zifuatazo zinaweza kujitokeza:

(i) Msimulizi na mhusika mwenzake wanaagana, pengine mhusika anakwenda ng'ambo kwa masomo. Ana furaha ya safari na huzuni kwa kuagana na rafiki.
(ii) Mzazi amekuwa na mwana mpotevu. Amerudi nyumbani akiwa amehasirika, pengine kwa ugonjwa. Msimulizi anashuhudia hisia za mzazi.
(ii) Mhusika anajiunga na kidato cha kwanza. Ana furaha ya kuanza maisha mapya na huzuni kwa kuaga nyumbani.
(iii) Bibi arusi anafurahia kupata mume, anahuzunikia ugeni wa hali, na kuacha kwao.
(iv) Mgonjwa amefanyiwa upasuaji. Ana huzuni kwa uchungu, na furaha kwa kupata tiba mwafaka.
(v) Msimulizi na rafiki yake wamekamilisha kidato cha nne, wana furaha ya kuhitimisha masomo yao na huzuni ya kuagana.
(vi) Msimulizi amemweleza mhusika mwenzake habari yenye kufurahisha na kuhuzunisha pia.
(vii) Mhusika amehusika katika ajali, ameumia lakini yu hai, anangojea matibabu.

**Tanbihi**

(i) Kisa kinaweza kusimuliwa katika nafsi ya kwanza, ya tatu, au mchanganyiko wa nafsi ya kwanza ya tatu, na hata ya pili.
(ii) Mtahiniwa, baada ya kuandika kauli ya kwanza, anaweza kutumia mbinu rejeshi, akarudi nyuma kuelezea hali ambayo ilisababisha hisia mseto za mhusika mwenzake.
(iii) Mtahiniwa, baada ya kauli ya kwanza anaweza kusimulia moja kwa moja kisa kinachofuata baada ya kutazamana huku. Yumkini anaweza kusimulia safari yake (msimulizi) baada ya kuagana na mhusika mwenzake.

## 4.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

1. (a)
   (i) Kufurahia / kunufaika kwa mandhari ya kupendeza
   (ii) Ushirikiano -babu na watoto, wanakijiji / kujaliana maslahi/kukuza ukarimu - kuombana vifaa kama vile unga na mboga
   (iii) Chakula cha kiasili
   (iv) Hamna misongamano
   (v) Kujuana
   (vi) Usalama
   (vii) Kufanya kazi ili kuufanyisha mwili mazoezi
   (viii) Kuepuka udhaifu / magonjwa yatokanayo na ulaji chakula hafifu
   (ix) Kuuzoesha mwili utendaji kazi - kujifunza ukakamavu. Babu anasema hamna wakati wa kulaza damu.

   6 x 1 = 6

   (b)
   (i) Msimulizi
   I Wingi wa magari kama ishara ya maendeleo
   II Uwezo wa kifedha uko juu
   II Wanaoishi huko kupata huduma za dharura kwa urahisi
   IV Usafiri kuwepo kila mahali wakati wowote

   3 x 1 = 3

   (ii) Babu
   I Maisha ya mji ni yenye kasi/kasi isiyoridhisha
   II Kutojuana / kutojaliana kwa wanajamii
   III Kufanya watu kutotambua usuli wao
   IV Kuteteresha mahusiano ya kijamii
   V Kupalilia uzembe / kutoushughulisha mwili
   VI Hutinga utekelezaji wa shughuli kwa sababu ya msongamano

   4 x 1 = 4

   (c) Kwenda kwa wakwe wako upate ndio wanakwenda uchi
   (i) Kwenda kwa mtu na kumpata ndipo anapofanya kosa; au
   (ii) Kwenda kwa mtu na kumpata hajajitayarisha; au
   (iii) Kwenda kwa mtu na kumkuta katika hali ya aibu.

   1x1 = 1

   (d) Niliona kisunzi
   (i) Niliona kizunguzungu
   (ii) Niliona masua
   (iii) Niliona kusulisuli

   1 x 1 = 1

2. (a) Kutofanya mazoezi husababisha:

   (i) Hatari ya kufa mapema
   (ii) Kukosa nguvu za kufanya kazi zinazohitaji nguvu
   (iii) Kusahau mambo kwa urahisi kwa kukosa kuchochea kuundwa kwa seli mpya
   (iv) Sehemu za ubongo kushindwa kujifunza mambo mapya

(v) Kushindwa kusuluhisha matatizo
(vi) Matatizo ya moyo kama vile kushindwa kupiga damu ili kuisambaza mwilini
(vii) Mwili kushindwa kupambana na magonjwa k.v. kisukari na shinikizo la damu
(viii) Mwili kushindwa kuchoma mafuta na kalori zisizohitajika / kuongezeka kwa uzani wa mwili
(ix) Kuupoka mwili majukumu/mahitaji yake ya kikaida . Mwili ulidhamiriwa ku fanya mazoezi.
(x) Kujikosesha fursa ya kuchochewa kufanya maamuzi na kusuluhisha matatizo / kuifanya akili kukosa uwezo wa kuibua suluhisho na maamuzi.

8 x 1 = 8
Mtiririko - alama 1
Jumla - alama 9

(b) (i) Mazoezi husaidia kujenga misuli inayowezesha kufanya kazi kwa muda mrefu bila kuchoka.
(ii) Mazoezi hasukama hewa yenye virutubisho na kuvisaidia viungo vya mwili kufanya kazi vyema zaidi.
(iii) Mazoezi husaidia kujengeka kwa mifupa.
(iv) Hukawiza kudhoofika kwa mifupa.
(v) Huimarisha mwili na kuufanya kunyumbuka.
(vi) Huleta utulivu wa kiakili.
(vii) Hudhibiti unyong'onyevu.
(viii) Hupalilia usingizi.
(ix) Ni muhimu kufanyisha mwili mazoezi ili kuupa hamu ya kufanya kazi.

5 x 1 = 5
Mtiririko - alama 1
Jumla - alama 6

3. (a) (i) /ng'/
(ii) /v/
(iii) /o/
(iv) /y/

$4 \times \frac{1}{2} = 2$

(b) Wa - nywe - sha - vyo alama 1/0

(c) Wafanyakazi wote **watatathminiwa** ili **kusuluhisha / tusuluhishe** matatizo hayo.
alama 2/0

(d) Ukihifadhi nafaka hiyo vizuri eneo hili litakuwa na chakula cha kutosha.
alama 2/0

(e) Mifano:
tu-li-u-chez-esh-a
tu-li-m-som-esh-a
tu-li-u-ig-iz-a
tu-li-li-end-esh-a
tu-li-ki-ugu-z-a

alama 2/0

(f) (i) Kama unataka kufaulu tia bidii.
(ii) Tuki ni mrefu **kama** babake.

(g) Mf (i) Nguo **ambazo zilinunuliwa** zitauzwa.
(ii) Matunda **yauzwayo sokoni** huwa mabivu.
(iii) Mto **uliofurika mwaka jana** ulitatiza usafiri.

**Tanbihi**
Mtahiniwa anaweza kutumia 'amba' au 'o' rejeshi.

alama 2/0

(h) Majumba hayo yalijengwa mbali na jiji lile. alama 1/0

(i) Mifano

(i) Kikosi cha wanahewa kingali hapa.
N KH/RH t E
(ii) Darasa la wanafunzi limekuwa kwetu.
N KH/RH E E

alama 2/0

(j) Viinilishe vingi vinapatikana (hupatikana/ vyapatikana) kwenye (katika) chakula kinachozalishwa kwa njia za kiasili. alama 1/0

(k) **Yeye** atazuru **huko**.
**Huyu** atazuru **kule**.
**Huyo** atazuru **huku**.
**Yule** atazuru **kule**.
**Yeye** atazuru **hii/ hizi**. alama 1/0

(l) "Basi mwanangu, akasema Daudi," hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia 'Vision 2030'. Wewe waonaje?"

$12 \times \frac{1}{4} = 3$

(m) (i) Beti alijishindia tuzo **baada ya /kabla ya** kushiriki katika utunzaji wa mazingira.
(ii) Beti alijishindia tuzo **kisha** akashiriki katika utunzaji wa mazingira.
(iii) Beti alijishindia tuzo **halafu** akashiriki katika utunzaji wa mazingira.
(iv) **Baada ya / kabla ya** Beti kushiriki katika utunzaji wa mazingira, alijishindia tuzo. alama 1/0


(n) (i) (a) Musau alituzwa **kwa** uaminifu wake.
(b) Hawa wamesifiwa **kwa** wema wao.
(c) Alijiua **kwa** pendo alilokuwa nalo kwake.
(d) Amefanikiwa **kwa** bidii yake.

alama 1/0


(ii) (a) Wake **kwa** waume walimshangilia.
(b) Wageni walipikiwa wali **kwa** samaki.

alama 1/0

(o)


S
KN
KT
N
T
S2/ S̄
KN
KT
TS
T
Mvua
ilinyesha
Ø
tulipokuwa
tukilima

**au**


S
KN
KT
N
T
S̄/S2
Mvua
ilinyesha
tulipokuwa tukilima

alama 2/0

(p) Siwa ilipuliziwa kwa Shaka na Malik. alama 2/0

(q) Kitendo cha kuiva kinasababishwa na kutiwa kapuni. alama 1

(r) (i) Mmomonyoko wa udongo unapozuiliwa mashamba hunawiri (yananawiri/ yanawiri).
(ii) Mmomonyoko wa udongo ukizuiliwa mashamba hunawiri (yananawiri/ yanawiri).
(iii) Mmomonyoko wa udongo uzuiliwapo mashamba hunawiri (yananawiri/ yanawiri).

alama 2 /0

(s) Sentensi idhihirishe maana zifuatazo:

fito (i) Vipande vya miti au vyuma virefu na vyembamba ambavyo hutumiwa kujengea nyumba.

(ii) Ada inayotolewa mwanafunzi anapoingia chuoni.

Vito (i) Mawe ya thamani k.v almasi yanayotumiwa kama pambo katika pete au mkufu. Pia johari.

(ii) Michezo ya watoto ya kuficha vitu na kuvitafuta.

Mfano: Hao hawakujua thamani ya vito vilivyotengeneza mkufu huo, wakauweka katikati ya miti ya kukatia fito za kujengea.

alama 2

(t) (i) Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo.
(ii) Kiserema hulima kikashinda jembe zima.
(iii) Pwagu hupata pwaguzi.

alama 1/0

(u) Mwenyewe akipenda kwa dhati
kiima chagizo

$2 \times \frac{1}{2} = 1$

(v) Sumile / simile

alama 1/0

(w) (i) Mvua isingalinyesha mazao yasingalipatikana.
(ii) Hazina asingefanya bidii asingefaulu maishani.
(iii) Kama Tunu hangekusaidia hungekamilisha kazi hiyo.

(x) (i) Kuwa joka la mdimu
(ii) Kufanya inda

alama 1/0

(y) (i) mfinyo
(ii) suke

$2 \times \frac{1}{2}$ = alama 1

4. (a) (i) Sajili ya kituo cha polisi
(ii) Mazungumzo kati ya polisi na mshukiwa

alama 2/0

(b) (i) Kuzingatia urasmi - *Sir*, afande
(ii) Matumizi ya msamiati maalum / istilahi za askari polisi - utafanyiwa *booking* vipi?
(iii) Kauli fupifupi - kwa vile ni mahojiano kati ya mshukiwa na polisi - Jina? Samwel Kibao
(iv) Lugha ya kuhoji - jina? Huna kitambulisho?
(v) Lugha ya kuamrisha - fanya upesi - (polisi)
(vi) Lugha ya unyenyekevu (mshukiwa) *Sir*, afande
(vii) Kuchanganya ndimi / msimbo - *booking, Sir*
(viii) Kukatwa kauli kwa mshukiwa na polisi - Naomba ... Naomba! Naomba!. Unaomba nini?
(ix) Toni kali ya kutisha (polisi). Usiniharibie muda wangu! Ingia ndani! Utakuwa mgeni wetu!

8 x 1 = 8

**Tanbihi**

**Lazima** mtahiniwa atoe mifano mwafaka kutoka kwenye kifungu. Asipotoa mfano asituzwe alama **yoyote**.

## 4.2.3 Kiswahili Paper 3 (102/3)

1. (a) (i) Mighani 1 x 1 = 1

(ii)
- (i) kinahusu shujaa - Jabari
- (ii) kuzaliiwa anashika mkuki
- (iii) kilio kuwa mngurumo
- (iv) nyota kuanguka
- (v) kuvuvumuka kabla hata ya kunyonyeshwa
- (vi) kuwaua maadui kwa konde
- (vii) ulimwengu kutetemeka na kutwaa giza
- (viii) Inahusu jamii iliyowahi kuishi Sule na Suna. $2 \times \frac{1}{2} = 1$

(iii)
- (i) Hutambulisha jamii - kila jamii huwa na shujaa wake. Kwa mfano Fumo Liyongo - Waswahili.
- (ii) Kutumiwa kama sifo, kuwasifu mashujaa wa jamii mahususi
- (iii) Kufunza ukakamavu/ujasiri. Mshujaa huwa na ujasiri. hupigana vita na kufikia ufanisi. Wanajamii wanaweza kuiga ukamavu huu.
- (iv) Kuhifadhi historia ya jamii kwa kuipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine/kuwajuza wanajamii kuhusu mashujaa wao/matukio katika jamii.
- (v) Kuhimiza uzalendo. Mashunjaa hujitolea kuzikomboa jamii zao, hivyo wanajamii wanaweza kuwaiga.
- (vi) Kuonya dhidi ya kupuuza mambo madogomadogo. Shujaa huangamia kwa kupuuza unafiki wa watu walio karibu naye.
- (vii) Kupitisha thamani za jamii kama vile stahamala.
- (viii) Kukuza ushirikiano kwa kuwajumuisha watu kusikiliza
- (ix) Wanajamii hupata nyenzo ya burudani.
- (x) Ni kumbukumbu ya mashujaa. Ni njia ya kuwaenzi.
- (xi) Utambaji wake hutumiwa kurithisha fani yenyewe ya utambaji.
- (xii) Kukuza lugha/kuwafunza vijana mbinu za kuwasilisha mawazo.
- (xiii) Utambaji wake ni njia bora ya kupitisha muda, badala ya kujihusisha na mambo yasiyo na faida.
- (xv) Ni nyenzo ya kukuza/kunoa kumbukumbu ya wanajamii kwani mtambaji sharti awe na kumbukumbu nzuri ili kukumbuka matukio.
- (xvi) Jamii huweza kuitumia kufunzia mbinuishi (mikakati ya kukabiliana na changamoto) kama vile namna ya kuepuka mitego au shambulizi.
- (xvii) Kuendeleza utamaduni wa jamii.

6 x 1 = alama 6

**Tanbihi**: Lazima afafanue ili kutuzwa alama 1

(b) Majigambo/kivugo 1 x 1

(i) Shuguli za kiuchumi
   (i) Usasi/uwindaji - kwenye misitu sikuwa na kifani
   (ii) Ufugaji - mafahali na mitamba $2 \times \frac{1}{2} = 1$
(ii) Shughuli za kijamii
   (i) Wizi wa mifugo - mafahali na mitamba akatukabidhi
   (ii) Uchezaji wa ngoma - ngomani kunipiku
   (iii) Upiganaji miereka - kwenye nyanja za michuano
   (iv) Ndoa - makoo kulilia nikaha $2 \times \frac{1}{2} = 1$

(iii) Ili kufanikisha uwalishaji wa majigambo, anayejigamba:
(i) Avae maleba yanayohusiana na anachojigambia.
(ii) Abadilishe toni na kidatu kulingana na hali anazosifia, ili kuondoa ukinaifu.
(iii) Arejelee mifano na hali halisi katika jamii ya hadhira yake ili aweze kuiteka.
(iv) Abebe zana/vifaa vinavyohusiana na anachojisifia. Kama ni usasi abebe zana za usasi.
(v) Awe mcheshi ili aweze kuichangaamsha hadhira, na kuzungumzia masuala mazito bila kukinaisha.
(vi) Aielewe vyema lugha ya hadhira yake ili aweze kufaragua kufanikisha uwasilishaji.
(vii) Awe mkakamvu kiasi cha kuweza kuzungumzia hata masuala nyeti katika jamii bila woga.
(viii) Aihusishe hadhira yake, pengine kwa kuulizia maswali ya balagha, ili kuteka usikvu wao.
(ix) Anaweza pia kubadilisha mtindo wa uwasilishaji kwa mfano, akaghani baadhi ya beti, na pengine kuimba baadhi.
(x) Aufahamu utamaduni wa hadhira yake ili kuepuka msamiati na ishara zinazoweza kuzua aibu na kutinga mawasiliano.
(xi) Atumie ishara/miondoko inayoafikiana na hali anayosifia.
(xii) Aigize hali anazojisifia. Kwa mfano anaweza kuigiza upiganaji miereka na uchezaji ngoma.
(xiii) Kufaragha.
(xix) Kuelewa hadhira. 5 x 1 = 5

(b) Umuhimu wa nyimbo katika utambaji wa ngano
Nyimbo:
(i) Huchangia kuifanya ngano iburudishe zaidi.
(ii) Husisitiza wazo (dhamira) ambalo mtambaji anakuza katika matini yake.
(iii) Ni kitulizo; kusaidia kuiondolea hadhira hisia za mhemeo, pengine kama ngano inahusu hali ya kusikitisha.
(iv) Ni njia ya kuondoa ukinaifu- ubadilishaji wa mtindo huwafanya wasikilizaji kufurahia utambaji zaidi.
(v) Hufumbata baadhi ya maudhui/migogoro katika ngano.

(vi) Huweza kutumiwa kufupisha usimulizi, ukajumuisha masuala, hivyo kupunguza baadhi ya matukio ya hadithini.

(vii) Ni njia ya fanani ya kuihusisha hadhira - anaweza kuitaka kushiriki katika uimbaji.

(viii) Hutumiwa kutenga matukio katika ngano. Kwa mfano, baada ya mgogoro fulani, shujaa katika ngano huweza kuimba kisha akachukua hatua tofauti na ya awali.

(ix) Huchochea hisia ambazo mtambaji ananuia kuzipata k.v. furaha, huzuni/huipa hadithi toni.

(x) Hutumiwa kusawiri/kujumuisha/tabia/sifa za baadhi ya wahusika katika ngano.

4 x 1 = 4

2. (a) (i) Maneno ya mwandishi/msimulizi kumhusu Nasaba Bora /kauli inarejelea hali aliyomo Nasaba Bora.

(ii) Ameisoma barua ambayo ameandikiwa na Lowela.

(iii) Barua imeletwa na DJ, nyumbani kwake Nasaba Bora.

(iv) Lowela anatishia kwamba Nasaba Bora asipowaachilia Amani na Imani atatoboa siri kuhusu kitoto chao ambacho Nasaba Bora alimpagazia ulezi Amani. Ndipo Nasaba Bora anashtuka.

4 x 1 = 4

**Tanbihi**; Dondoo limetolewa uk .106

(b) (i) Nasaba Bora anawadhulumu raia, anachukua shamba la Chichiri Hamadi, baadaye anakuja kulipoteza shamba hili.

(ii) Mahusiano yake ya kimapenzi na Lowela yanamsababishia Lowela mimba ya mapema. Nasaba Bora analazimika kumpagaza Amani kitoto akilee, kwa kutotaka kujiaibisha.

(iii) Wivu wake kwa nduguye Majisifu unamfanya kumwonea kinyongo na kukuza mgogoro zaidi kati yao.

(iv) Uchu wake wa kimwili unamfanya kumpenda msichana mlemavu na baadaye kuhizika anapogundua kwamba msichana ni mlemavu.

(v) Kiburi kinamfanya kutobadilisha uongozi wake mbaya. Anaishia kuzikwa kwa fedheha. Askari wanakataa kufyatua mizinga.

(vi) Itikadi inayoongozwa na mawazo finyu ya kijinga inamfanya kutonadhifisha maskani yake. Kasri lake linaishia kuwa la kukirihisha.

(vii) Anahifadhi hatimiliki mbilimbili za mashamba bila kuwazia matokeo yake. Anakuja kuaibika Amani anapomwambia ampe hatimiliki hizo.

(viii) Ubahili wake unamfanya kutolifanyia ukarabati gari lake; lenyewe linaishia kuwa la kusukumwa na kumfedhehesha.

(ix) Uamuzi wake wa kumpakaza Amani kitoto unaishia kukifanya kitoto chake - Uhuru - kufa.

(x) Ufisadi wake unamfanya kukataliwa na mwanawe Madhubuti. Madhubuti anaungana na Amani kuupindua uongozi wa Nasaba Bora.

(xi) Wepesi wake wa kupapia kutoa uamuzi kwamba mke anamwendea kinyume na Amani unasababisha kusarambatika kwa ndoa yake. Anamtaliki mkwe bila ya ithibati tosha ya ukosefu wa uaminifu.

(xii) Uhusiano wake na Lowela unaishia kumsababishia mwanawe Mashaka wehu.

(xiii) Dhuluma yake kwa raia, inawafanya raia kumsahau kabisa baada ya kifo chake. Jina lake lilifutwa katika chochote kilichojulikana kwalo huko Tomoko (uk. 160).

(xv) Kugunduliwa kwa ufisadi wa Nasaba Bora kunamfanya kutoweza kukabiliana na hali yake mpya. Anaondoka Sokomoko na baadaye kujiua.

(xvi) Badala ya kurekebisha hali, anajiua na kujiumbua, mazishi yake yanahudhuriwa na wachache.

(xvii) Anaendeleza ufisadi katika Wizara ya Ardhi na Makao na kuishia kufutwa kazi.

(xviii) Wizi wa pesa zilizotengewa ujenzi wa hospitali unasababisha kujenga zahanati tu; yeye na raia wa Sokomoko wanakosa huduma bora zaidi za afya.

(xix) Kuwafungia Amani na Imani kunamfanya atishwe na Lowela na kusababishiwa fadhaa - moyo unampapa.

(xx) Kumfungia Amani kunamkosesha mfanyakazi wa kuwakama ng'ombe; chai ya mkandaa inaandaliwa.

(xxi) Dhuluma anayoitendea familia ya Imani inamfanya kutishiwa kuuawa na Oscar.

(xxii) Kutofuata mafundisho ya babake kunawafanya, yeye na Majisifu kutohusiana vyema kama ndugu.

(xxiii) Kutomtambua Matuko Weye kunamfanya kufedheheshwa Siku ya Wazelendo.

(xxiv) Uhusiano wa kimapenzi na Lowela - Lowela anapata mimba, Nasaba Bora analazimika kuwapagaza Amani na Imani kitoto wamlelelee.

(xxv) Uhusiano wake na Lowela unasababisha kusaambaratika kwa ndoa. Mapenzi yao yanavunjika. Hawana mwamana. Hata Zuhura anawahusudu wanawake wanaovaa rinda moja na ambao wamo pamoja na waume wao.

8 x 2 = 16
Udhaifu - 1
Hasara - 1

**Tanbihi**

**Sharti** mtahiniwa abainishe:

(i) Kosa, udhaifu au mapuuza ya Nasaba Bora

(ii) Namna udhaifu/kosa hilo lilivyomfanya kuhasirika yeye mwenyewe au yeye na wengine wanaomtegemea au wanaohusiana naye.

3. (a) Imani amewajibika kwani:

(i) Anaposhauriwa na Amani dhidi ya kujiua anakubali.

(ii) Hata anapaoambiwa na DJ asiyanywe maji ya mto Kiberenge haghairi nia, anayanywa na kuubadilisha mtazamo wa Watomoko kuwa ni mwiko kuyanywa maji haya.

(iii) Anaishi na Amani katika kibanda kimoja bila kukiuka mipaka ya uhusiano wao.

(iv) Anamsaidia Amani kumlea Uhuru.

(v) Hata askari wanapomtaka kuhudhuria mkutano wa Mtemi, anashikilia msimamo wake, anakataa.

(vi) Anakataa kuamini tetesi kuwa Amani na Bi Zuhura wana uhusiano. Anamwamini Amani.

(viii) Anawalea watoto walemavu wa Majisifu bila ubaguzi.

(ix) Anawakosoa wanakijiji wa Baraka kwa kuufumbia macho ukatili wa viongozi. Analalamikia hali yao ya kutotaka hata kuonekana hapo mwao Imani baada ya kuchomwa kwa nyumba yao.

(x) Anamtetea mama yake pale anapopigwa na askari.

(xi) Anamsuta Majisifu kwa kuendeleza wizi wa mawazo, anamkashifu kwa kuiba mswada wa Amani.

(xii) Anafanya kazi yake kwa bidii; anafanya kazi nyingi na ngumu nyumbani mwa Majisifu bila kulalamika.

(xiii) Hatoi nje siri za unyumba za Majisifu.

(xiv) Anamwadilisha nduguge Oscar kambona. Anamfanya kubadili msimamo wake wa kulipiza kisasi kwa Nasaba Bora. Anafanikisha kutangamana tena kwa familia yao kwa kumshawishi Oscar Kambona arudi nyumbani wasaidiane kumtunza ndugu yao (Chwechwe Makweche)

(xv) Anawajibika kuituuza mali ya familia yake. Hata mama yake anapouawa, yeye haondoki hapo nyumbani kama afanyavyo nduguge Oscar, anabaki pale hadi anapovunjikiwa zaidi- nyumba yao inachomwa, naye kunusurika kifo.

(xvi) Anamwonya Amani dhidi ya ubaguzi wa kijinsia. Anamwambia asimweke pembeni kama tanbihi katika riwaya yake.

(xvii) Anamuuguza Amani pale pa Majisifu.

(xviii) Anamwonya Majisifu dhidi ya kuingilia uhuru wa mtu binafsi. Anamsuta kwa kusoma barua yake (uk 142).

10 x 1 = 10

(b) Mwafrika hajakomaa·kwani:

(i) Badala ya Nasaba Bora kuyatunza mazingira anaendeleza uharibifu kwa kutonadhifisha kasri lake.

(ii) Viongozi wa Kiafrika wanarithi mfumo wa kikoloni na kuuendeleza badala ya kuubadilisha. Tunaambiwa kuwa Nasaba Bora alikuwa miongoni mwa Waafrika waliojua mizungu ya kurithi uluwa na mali baada ya kuondoka kwa Mzungu/unyakuzi wa ardhi.

(iii) Nasaba Bora anaendeleza ufisadi katika Wizara ya Ardhi na Makao na kuishia kujisababishia kufutwa kazi.

(iv) Nasaba Bora hajakomaa kimawazo. Anashindwa kuona umuhimu wa kuyachanja majibwa yake.

(v) Majisifu, pamoja na kisomo chake, anashindwa kuona umuhimu wa kuwatunza watoto wake walemavu.

(vi) Majisifu anashindwa kuwajibikia kazi yake. Anakosa kuhudhuria madarasa yake.

(vii) Nasaba Bora na Majisifu wanashindwa kufuata mafundisho ya kidini waliyorithishwa na baba yao. Wanashindwa hata kuhusiana vyema kama ndugu.

(viii) Fao anakosa kujidhibiti kama mtaalamu. Anahusiana kimapenzi na mwanafunzi wake na kumtunga mimba.

(ix) Wazazi wa Fao wanaendeleza upujufu wa thamani ya mitihani, wanamlipia Fao kufanyiwa mtihani.

(x) Mwafrika anashindwa hata kutunza rasilimali aliyoachiwa na Mzungu. Nasaba Bora anayaachia ovyo makochi nyumbani mwake.

(xi) Nasaba Bora anaonyesha kutokomaa kwa kuhusiana kimapenzi na Lowela na mwishowe kusababisha kuwehuka kwa bintiye Mashaka.

(xii) Wasomi kama vile Majisifu badala ya kuendeleza utafiti, wanaufifilisha kwa kuiba miswada - anamwibia Amani.

(xiii) Nasaba Bora, badala ya kupigana na ukatili, ndiye anayeuendeleza. Anampiga Amani bila ithibati tosha kwamba anamwendea kinyume.

(xiv) Uongozi unashindwa kuwahakikishia raia usalama. Nasaba Bora anawatuma watu kuchoma nyumba ya akina Imani.

(xv) Viongozi wanaendeleza dhuluma kwa waliopigania uhuru. Matuko Weye hajafidiwa kwa athari za Vita vya Dunia.

(xvi) Viongozi wanafifilisha vipawa vya vijana badala ya kuvikuza. Chwechwe Makweche licha ya kuiletea nchi sifa, anatelekezwa anapoumia mguu.

(xvii) Viongozi wanaendeleza ukiukaji wa haki za watoto. Nasaba Bora anampagaza Amani malezi ya Uhuru, anakitupa kitoto hicho mlangoni mwa kibanda cha Amani, licha ya baridi kali.

(xviii) Nasaba Bora anaendeleza matumizi mabaya ya mali ya umma. Anawataka raia kutoa pesa ampeleke mwanawe Madhubuti kwa masomo ng'ambo.

(xix) Balozi, badala ya kumshauri vyema na kumkosoa Nasaba Bora, anamsifu kiongo, anasema kwamba Tomoko ina viongozi mashujaa wanaojali masilahi ya raia.

(xx) Uongozi wa zahanati unawatelekeza wagonjwa. DJ anatelekezwa hadi anatoroka kutafuta matibabu badalia.

(xxi) Viongozi wanaendeleza udikteta; wanaongoza kwa vitisho. Tunaambiwa kwamba anenalo Nasaba Bora ndilo sheria.

(xxii) Wakuu wa mashirika ya kitaifa wanaendelea kuwasifu viongozi kupitia vyombo vya habari badala ya kuwakosoa. Majisifu alihakikisha kuwa jina la Nasaba Bora limetokea katika gazeti la Tomoko leo.

(xxiii) Majisifu anashindwa kujidhibiti kama mwanataaluma; analewa hadi analala mitaroni.

(xxiv) Viongozi wanabadhiri pesa zilizotengewa ujenzi wa hospitali na kusababisha kujengwa kwa zahanati tu. Wanaathiri vibaya utoaji wa huduma za afya.

(xxv) Viongozi wanatumia pesa zilizokusudiwa udhamini wa elimu ya watoto maskini kuwapeleka watoto wa familia tajiri kama vile Fao na Madhubuti kwa

masomo ng'ambo.

(xxvi) Viongozi wanapuuza afya ya wanyama wa kufugwa. Nasaba Bora hayachanji majibwa yake.

(xxvii) Nasaba Bora anakosa uwajibikaji kwa raia. Anampita mama anayejifungulia njiani.

(xxviii) Viongozi kuendeleza mauaji - chichiri na mame/mani.

(xxix) Viongozi kuwafungia raia bila hatia. Amani - uchochezi, Imani na Amani, Yusufu. Matuko Weye.

(xxx) Majisifu ni msomi lakini anashindwa kujiandalia mhadhara, uwasilishaji wake unatibuka kule Wangwani. 10 x 1 = 10

**Tanbihi**: Dondoo limetolewa uk 124.

4. (a) (i) Ni maneno ya Diwani III (Bw. Kheri)

(ii) Anamwambia Siki.

(iii) Wamo nyumbani mwa Diwani III.

(iv) Siki amekuja kumwona Diwani III.

(v) Diwani III anamwambia Siki kwamba kuna mikutano ambayo yeye Diwani III hashirikishwi lakini anaamrishwa kutekeleza yaliyoafikiwa katika mikutanao hiyo.

(vi) Siki anamwambia kwamba anastahili kukataa kutekeleza, ndipo Diwani III anasema haya.

**Tanbihi**: Dondoo limetolewa uk. 46 4 x 1 = 4

(i) Tashbihi - kushindana naye ni kama kushindana na ndovu.

(ii) Sitiari - utapasuka - utaumia/utaathirika vibaya.

(iii) Taswira - mnyonge kushindana na mwenye nguvu.

1 x 2 = 2

Kutaja - 1
Mfano - 1

(b) (i) Meya ana uwezo wa kutoa ahadi za uongo na kuaminika. Anadanganya kwamba dawa zimeagizwa, zi njiani na hali sivyo.

(ii) Meya ana washauri wengi ambao wanamsikiliza. Raia/mtu mmoja tu hawezi kushinda.

(iii) Matumizi ya vyombo vya dola. Watu wanapogoma au kulalamikia haki wanatawanywa na askari.

(iv) Washauri wengine wa Meya kama vile mhubiri na Bili wana uhitaji na tamaa, hivyo hawawezi kumpinga Meya.

(v) Meya anawatenga washauri wanaopigania haki (k.v. Diwani) za wanyonge, kwa kudadisi mambo, hivyo anaishia kutoa uamuzi anaopendelea yeye.

(vi) Ana mamlaka ya kisheria (Mayors Act na Riot Act) ambayo yanampa idhini ya kumchukulia hatua yeyote anayempinga. Meya anayatumia mamlaka haya vibaya/kujidumisha uongozini.

(vii) Uwajibikaji wa pamoja unawafanya hata madiwani wanaoweza kumpinga Meya kutofanikiwa, kwani wale wengi huwa wamelitia sahihi alitakalo Meya.

(viii) Hata Meya akiwadhulumu raia, wanamrudisha uongozini kwa kumpigia kura.

(ix) Meya hana upinzani kutoka kwa wasomi kwani wanachelea kujihusisha na siasa. Siki anaiona siasa kuwa mchezo mchafu.

(x) Meya anatumia vitisho. Anadai kwamba wapo wasio na kazi, hivyo wataajiriwa.

(xi) Anabuni kamati nyingi na kuwatia viongozi awatakao (wenye ushawishi) ili wamuunge mkono. (Katiba imempa mamlaka hayo)

(xii) Ana mamlaka ya kutumia pesa/kupangia matumizi ya pesa au rasilimali za baraza. Anawaongezea mshahara walinda usalama ili waendelee kuulinda uongozi wake dhidi ya wapinzani. Anampa mhubiri sadaka ili amuunge mkono. Anawapeleka watoto wake ng'ambo ili kuepuka elimu duni.

(xiii) Ana nyenzo za kushawishi. Anatumia vyombo vya habari kueneza propaganda kuusifu na kuuondoa uongozi wake lawamani na kuibua hisia za kizalendo. Anataka idhaa ya kitaifa icheze nyimbo za kizalendo.

(xiv) Anawaondoa wanakandarasi wa awali ambao anahofia watapinga mipango yake/ana uwezo wa kuangamiza upinzani.

(xv) Hata mji unapojaa uvundo yeye ana wafanyakazi kama vile Dida wa kunadhifisha kwake.

(xvi) Ndiye anayeamua kuhusu mikutano ya kuamulia masuala ya kisera, hivyo ana uwezo wa kuwatenga wapinzani wake kama vile Diwani III.

(xvii) Ndiye pekee mwenye jukumu la kuamua kuhusiana na matumizi ya viwanja vya umma hivyo anawagawia wanaomuunga mkono.

(xviii) Hata akitenda uhalifu ana nyenzo za kuuficha. Diwani (1) anaotoka na fimbo kisha kusemekana kwamba kumetokea vurugu fimbo ikaibiwa.

7 x 2 = 14

5. (a) (i) Ufisadi/kuhonga - Kummegea - kumgawia

1 x 2 = 2

**Tanbihi**: Dondoo limetolewa nk.27

(ii)

(i) Meya anaidhinisha kuongezewa mishahara kwa madiwani ili wamuunge mkono. Hazina ya baraza inamomonyolewa zaidi. Madiwani hawampi ushauri wa kweli - uongozi unaanguka.

(ii) Meya akamgawia Bili viwanja vinne. Bili anaishia kumpa ushauri wa kupotosha. Bili anaiba fimbo ya Meya.

(iii) Meya anaifisidi hazina ya baraza kwa kumpeleka Bili na familia yake kwa burudani.

(iv) Bili anamshauri Meya amwambie mwanakandarasi alishtaki baraza ili apewe fidia kwa kukatizwa kwa kandarasi Meya atapate fungu lake pia. Analifukarisha baraza.

(v) Meya anaunda kamati nyingi ili kuwahonga madiwani wanaomuunga mkono. Anaishia kushauriwa kufanya maamuzi yasiyo ya busara - anakataa kuwasikiliza wafanyakazi, mji unajaa uvundo, wageni wanaahirisha safari, uongozi wa Meya unaanguka.

(vi) Meya anamhonga mhubiri kwa sadaka ili aendelee kumwombea. Mhubiri anashindwa kumkosoa Meya, uongozi unaanguka.

(vii) Meya anamlipa Bili kwa huduma ambayo kwa kweli hajatoa. Huu unakuwa mzigo kwa hazina ya baraza.

(viii) Raia wanachukua hongo kutoka kwa viongozi, wanawachagua na kuendeleza uongozi mbaya. Meya anamwambia Siki kwamba hata akitaka uongozi mara nne, tano na sita atapewa, kwani ana akili na uwezo wa ushawishi.

(ix) Ufisadi unamfanya Meya kumshirikisha Bili katika maamuzi muhimu ya Baraza, na hali Bili si mfanyakazi wa Baraza. Bili anaishia kumpotosha Meya.

(x) Meya anaidhinisha Diwani I na Diwani II kulipwa overtime na hali hawajafanya lolote. Anaishia kumpa Bili upenyu wa kushauri wauze fimbo ya Meya.

(xi) Ufisadi unamfanya Diwani I (Bwana Usalama ) kufanikisha wizi wa fimbo ya Meya. Anatoka nayo, kisha anatangaza kwamba kulitokea rabsha ikaibwa.

(xii) Ufisadi unawafanya Meya, Diwani I, Diwani II na Bili kutotoa siri kuhusu njama ya kuiba fimbo ya Meya. Baraza linapata hasara.

(xiii) Meya anaidhinisha kutotozwa kodi kwa madiwani kwa kutaka wamuunge mkono. Hili linalinyima baraza pato na kuzidisha nakisi ya fedha.

(xiv) Meya anaifisidi mali ya umma kwa kumpeleka mkewe kujifungulia ng'ambo na wanawe pia kusomea ng'ambo. Anakosa kuboresha huduma za afya na elimu.

(xv) Meya/Baraza linashughulikia masilahi ya kiafya ya madiwani kwa kutaka kuungwa mkono, na kuwapuuza wanyonge. Zahanati inakosa dawa, raia wanakufa; mf. Dadavuo.

(xvi) Meya anampa mhazili nafasi ya kazi licha ya kuwa hastahili. Anawanyima nafasi hiyo wanaostahili, k.v. wasomi.

(xvii) Diwani I na II wanamuunga Meya mkono kwa yote anayotaka ili wafaidi. Wanampotosha, uongozi unaanguka. 8 x 1 = 8

(b) Vyombo vya usalama vinaendeleza uongozi kwa namna zifuatazo:

(i) Askari wanatawanya wafanyakazi wanapogoma, hivyo kudhibiti upinzani.

(ii) Askari wanawatisha na kuwashinikiza watu wafanyakazi wakae nyumbani ili baraza lisipate picha mbaya ya ukosefu wa usalama.

(iii) Madiwani wanatumiwa kupanga mikakati ya kumdumisha Meya mamlakani. Diwani I kwa mfano, anaendeleza propaganda kuhusu kujitolea kwa baraza kutetea demokrasia.

(iv) Meya, ambaye anastahili kuwahakikishia raia usalama, unaidhinisha kuundwa kwa kamati zinazoongozwa na madiwani wenye ushawishi mkubwa. Hali

hii inapuguza pingamizi.

(v) Kinara wa usalama, (Diwani I) anamshauri Bwana Uhusiano Mwema kuandaa tamasha kwa vijana ili kupalilia uzalendo kwa uongozi na Meya.

(vi) Madiwani wanatumia vyombo vya habari kuimarisha uzalendo. Diwali II anasema kwamba mashindano ya vijana yatapeperushwa moja kwa moja kupitia vyombo vya habari.

(vii) Katiba, inayopaswa kuhakikisha usalama inampa Meya mamlaka ya kukabiliana na wanaotetea haki, hivyo kumdumisha mamlakani.

(viii) Madiwani na walinda usalama wanaostahili kulinda haki za raia wanaongezewa mshahara ili kuendelea kumuunga Meya mkono.

(ix) Baraza linamtenga Diwani III katika maamuzi mabaya ambayo linafanya ili kukinga dhidi ya pingamizi.

(x) Askari wa baraza wanalinda masilahi ya Meya. Hata wanaposikia kelele za jadhba ya maombi wanakuja mbio kumhudumia.

(xi) Mkuu wa usalama (Diwani I) anatumia vitisho (kuwafuta kazi) ili kuwadhibiti wafanyakazi wasigome.

(xiv) Diwani I anatoka na fimbo ya Meya afisini na kudai kuwa kulitokea vurugu ikaibwa. Hili linawatoa viongozi lawamani.

(xv) Meya anapokisia kwamba walinda usalama wakitumia nguvu watasababisha upinzani anaamuru kwamba hataki watu wauawe (uk.19). Hii ni njia ya kujidumisha mamlakani. 10 x 1 = 10

6. (a) (i) Mwenye tumaini/tamaa - kubwa hamu

(ii) Mwenye bidii - alfajiri na mapema, kutokwa na jasho

(iii) Anayeyafurahia mandhari - anapotembea anasikiliza videge...

(iv) Mtulivu - kuna siri gani inayomliwaza?

(v) Aliyedhulumiwa - soko la dunia lamkaba koo.

(vi) Anayesagika kwa kazi ngumu kuwafaidi wenye tamaa-ayalamia matumbo ya waroho.

(vii) Aliyeridhika - kuna jambo gani?

4 x 1 = 4

(b) (i) Inkisari - babuze - babu zake

(ii) Kufinyanga sarufi/miundo ngeu ya kisintaksia - kubwa hamu - hamu kubwa

2 x 1 = 2

(c) (i) Taswira **mnuso**/harufu - rihi ya maua

(ii) Taswira **mguso** - kumpapasa, kumbusu miguu

(iii) Taswira ya **usikivu** - anasikiliza videge

(iv) Taswira ya **mwendo** - yeye <u>kuendelea</u> kwa furaha.

3 x 1 = 3

(d) Maswali ya balagha yametumiwa:

(i) Kudadisi hali - kuna siri gani inayomliwaza? Kuna jambo gani linamridhisha? Au ni kujua au kutojua?

(ii) Kuonyesha hali ya kinyume, kutokubaliana na jambo Furaha ya mtu ni furaha gani, katika dunia inayomhini?

(iii) Kuzindua - furaha ya mtu ni furaha gani katika dunia inayomhini?

2 x 1 = 2

(e) (i) Tashhisi - umande kumbusu, miti kumpapasa, kumtoa matongo, upepo kumpepea

(ii) Kinaya - nafsineni inafurahi ilhali dunia inaihini.

(iii) Tashbihi- kama mtu aliye na kubwa hamu

3 x 1 = 3

(f) (i) Toni ya uchungu - Furaha ya mtu ni furaha gani katika dunia inayomhini?

(ii) Toni ya kuajabia/kushangazwa na jambo - kuna jambo gani linamridhisha?

(iii) Kuhuzunisha/masikitiko/kuhurumia - laiti angalijua.

1 x 2 = 2
kutaja - 1
kueleza - 1

(g) Nafsineni

(i) mtetezi wa haki/aliyezinduka/anayelalamikia dhuluma ya wanyonge.

(ii) mtu anayemtazama mkulima akipita.

1 x 1= 1

(h) (i) Shairi lina beti tatu.

(ii) Kila ubeti una idadi tofauti ya mishororo na beti nyingine.

(iii) Kila mshororo una kipande kimoja.

(iv) Shairi halina mpangilio maalum wa vina.

(v) Idadi ya mizani katika mishororo inatofautiana. 3 x 1 =3

7. (a) (i) Dhamira ya mtunzi ni kuonyesha kuwa kazi ni shughuli muhimu ila haiwezi kuzingatiwa zaidi ya afya.

(ii) Kuonyesha kuwa ipo haja ya kuipa afya kipaumbele kwa kuvikataa vitisho vya wenye kazi/waajiri.

(iii) Kuonyesha dhuluma wanazofanyiwa wafanyakazi- vitisho pamwe kelele

(iv) Kuukosoa uongozi dhalimu- kufutwa sikawi.

(v) Kuzindua wafanyakazi. 4 x 1 = 4

(b) Hoja zifuatazo kujadiliwa:

(i) Shairi linatumia Kiswahili (lahaja) sanifu.
(ii) Kuna matumizi ya sitiari - si gurudumu mwili.
(iii) Uhaishaji/tashhisi - ugonjwa umepewa sifa ya kutenda-mwili kuudhili
(iv) Matumizi ya nahau - viraka kuutia (ub.3)
(v) Matumizi ya inkisari - huwezi - hauwezi, ngeushuruti - ningeushuruti, sikawi - sikawii, kivipichakiko - ukivipachiko.
(vi) Urudiaji wa maneno - kila mshororo unaishia kwa neno: mwili.
(vii) Udondoshaji wa neno - vitisho, pamwe kelele - vitisho pamwe na.
(viii) Tabdila - utimile - utimie.
(ix) Mazida - ukaungilika - ukaungika.

4 x 2 = 8

kutaja 1
mfano 1

(c) Toni ya:
(i) hasira - si gurundumu mwili
(ii) ukali - sihofu
(iii) machungu - wauma mwili
(iv) kukashifu - vitisho pamwe kelele

1 x 2 = 2

kutaja 1
mfano 1

(d) Mwenye kazi/mwajiri

1 x 1= 1

(e) Ukawafi - vipande vitatu katika kila mshororo.
kutaja 1
mfano 1

1 x 2

(f) Mimi kwa hakika ninaithamini kazi kwa akili na mwili isipokuwa siamimi kwamba inafaa kuteseka kwa kila hali. Hasa ugonjwa unapohusika kutumia nguvu hakuwezi kunitisha/siwezi kuogopa kutumia nguvu kujitetea. 3 x 1 = 3

8. (a) (i) (i) Maneno haya yalisemwa na Bimkubwa aliyemlea Sudi.
(ii) Alikuwa akiwaambia Sudi na mtumishi wake Bi Kudura.
(iii) Walikuwa nyumbani kwa Bimkubwa alikoishi na Sudi.

(iv) Ni baada ya Bimkubwa kutambua kwamba Sudi alikuwa mtoto wake Bi Kudura.
(v) Bi Kudura alimweleza Bimkumbwa namna aliyvomtupa mwanawe pipani.
(vi) Bimkubwa alijitolea kumfichulia Sudi siri hii na kuwataka wote wasameheane.

4 x 1 = 4

**Tanbihi** - dondoo limetolewa u.k. 118

(ii) Umuhimu wa hotuba ya Bimkubwa.

(i) Imemfumbulia Sudi fumbo kubwa alilotaka kulifumbua - alitamani kumjua babake na asili yake.
(ii) Kufichua udanganyifu wa Bimkubwa kuhusu Sudi. Kila wakati alipoulizwa na Sudi alikokuwa babake alimdanganya alifariki na kumwacha akiwa na mimba ya Sudi.
(iii) Kufichua siri ya namna Bimkubwa alivyomwokoa Sudi.
(iv) Kusawiri suala la uanaharamu - changamoto za kupata mtoto nje ya ndoa.
(v) Kuonyesha maudhui ya utu. Bimkubwa alimlea Sudi na kumsomesha kama mwanawe wa kuzaa.
(vi) Kuonyesha uwajibikaji - Bimkubwa kumlinda na kumtunza mwana aliyemwokota kama mtoto wake wa kuzaa.
(vii) Kuonyesha kwamba ni muhimu kukiri makosa, Bimkubwa anakiri alimdanganya Sudi lakini kwa kutaka aishi kwa furaha.
(viii) Kusisitiza umuhimu wa kuomba msamaha na kusameheana kwa dhati.
(ix) Kuonyesha busara ya Bimkubwa. Bimkubwa alikuwa amemwandikia Sudi mwanawe nyumba walimokuwa wakiishi na baada ya kufichua siri aliahidi kuhama na kuwaachia pamoja na Bi Kudura.
(x) Kuchimuza uozo wa kijamii. Bi Kudura alimtupa mwanawe.
(xi) Kuonyesha suala la haki za watoto - Bimkubwa kumlea Sudi baada ya kumwokoa.
(xii) Kimuundo ni kitulizo. Suluhisho la mgogoro wa hadithini linachimuzwa pale tunapoona maridhiano ya mwana na mama, na kudokezewa mkondo wa maisha ya baadaye ya Bimkubwa.
(xiii) Kuendeleza maudhui ya elimu. Sudi amesoma hadi chuo kikuu.
(xiv) Kuonyesha utu na uwajibikaji wa Sudi. Anamtunza vyema Bimkubwa.
(xv) Kuonyesha bidii ya Sudi. Anasoma hadi chuo kikuu.

8 x 1 = 8

(b) (i) Msimulizi kuwazia kwamba kwa vile Aziza hakusoma, hatakuwa mjuaji, atakuja kumdhibiti. Inatokea kwamba Aziza ndiye anayemdhibiti.

(ii) Msimulizi anaikashifu tabia ya Fedhele; kuwa yu nje usiku na hali msimulizi yu palepale nje wakati huo.

(iii) Msimulizi amesoma, na hali anafungwa na mawazo ya kizamani. Anamkashifu Fedhele na rafiki yake kwa kuandamana na kijana wa kiume.

(iv) Ni Kinaya kwamba Msimulizi anawaza kwamba waliosoma ndio wenye utambuzi, lakini anakuja kugundua kwamba Aziza ana utambuzi wake mwenyewe ulioshinda wa wale waliosoma.

(v) Ni Kinaya kwamba Msimulizi anataka kumtia Aziza mjini/lakini hataki Aziza aambukizwe mambo ya mji(afanye wafanyavyo wana mji).

(vi) Msimulizi alitaka kumfunza Aziza maisha ya kistaarabu lakini Aziza anaishia kumfunza kuwa mtu asiyefanya kazi si mume.

(vii) Ni kinaya kwa waliosoma kungojea kujituma kwenye kazi duni kama vile uboi, huku wakidharau kazi kama vile ukwezi ambazo zingewaimarisha.

(viii) Msimulizi kasoma, ila Aziza ana mawazo mapevu kumshinda. Hata anahisi kwamba Aziza kamzuga.

(ix) Msimulizi anakataa kumwoa Seluwa kwa sababu ya kuwa kidomo, baadaye anakuja kumwoa Aziza ambaye anamdhbiti kwa maneno.

(x) Inatarajiwa kwamba Aziza anapoolewa atafuata utamaduni wa familia ya mume, lakini anashikilia utamaduni wa kwao.

(xi) Msimulizi anakashifu kanzu fupi ya Fedhele na pia hapendezwi na wanaojigubika k.v. Salma.

(xii) Msimulizi hataki kumwoa mwanamke aliyestaarabika kwa vile ndoa zao zimesambaratika ilhali yake inaishia kusambaratika na hali mkewe hajastaarabika.

8 x 1 = 8